




Selemeng
anawapenda paka.
Kuna paka wengi
nyumbani kwake.



Selemeng ana paka
mmoja mweusi. Paka
huyu anakula nyama
nyingi.



Selemeng vilevile ana
paka mmoja mnono.
Paka huyu hula kila
kitu.




Paka wa tatu, alipanda
mtini na akakwama
huko.



Selemeng alimfuata
paka akakwama naye
mtini. Mamake
Selemeng alilazimika
kumsaidia kushuka
chini.



Selemeng pia ana paka
wawili wavivu.
Wanalala nje ya
nyumba wakiota jua
mchana kutwa.




Selemeng vilevile, ana
paka watatu wanao
shughuli nyingi. Usiku
wanawashika panya
jikoni.



Selemeng ana mbwa
anayeitwa Lirafi. Lirafi
ana huzuni kwa
sababu hana rafiki.




Paka wa Selemeng
hawampendi Lirafi.
Wanapomfukuza, Lirafi
anatoroka nyumbani.



Selemeng anapompata
Lirafi, anamrudisha
nyumbani. Paka
hawfurahi Lirafi
anaporejeshwa.
Hawataki kumwona
tena.



Selemeng ana paka
wangapi?



Selemeng ana mbwa
wangapi? Lirafi yuko
wapi sasa?

Nyumbani kwenu kuna paka wangapi?
Je, mna mbwa nyumbani kwenu?

